BUKOBA HOPE LUTHERAN SECONDARY SCHOOL (BUHOLUSE)
ELCT - NORTH WESTERN DIOCESE
P.O. Box 1425, Bukoba, Tanzania; **Phone**: +255 754 264 200/+255 28 222 0027
**Email**: bhl.nwdelct@gmail.com **Website**: www.bukobahopelctnwd.ac.tz
**Motto:** Where Everyone is in Christ, Everyone Wins

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026

**(Ukipata fomu hii mtandaoni, utaprinti nyuma na mbele ukr. 6-9. Zilizobaki ni hiari)**

**Mpendwa mwanetu: ………………………………………………………………………………**

## 1.0 UTANGULIZI

**Tunafurahi kukujulisha kuwa unazo sifa na umechaguliwa kujiunga Kidato cha I mwaka 2026 katika Shule ya Sekondari Bukoba Hope Lutheran. Tunapokea mtoto wa dini na kabila lolote. Hongera sana. Mungu amekujalia kuwa mwanafamilia inayoongozwa Kikristo kweli. Sisi ni Familia ya Washindi maana wanetu hushinda Kitabia na Kitaaluma. Wanetu huitana Kaka au Dada bila kujali umri (ni kama neno Ndugu). Ninahisi umesikia mazuri haya, ukatuchagua. Basi, ninakuomba uripoti shuleni tarehe 03/01/2026 Jumamosi. Muda ni tangu saa 1.30 asubuhi. Tuko kazini hata siku za mapumziko na usiku. Masomo yataanza 05/01/2026. Hatusubiri watakaochelewa. Ibada nzuri sana ya ufunguzi ni tarehe 04/01/2026.**

**Wazazi wakisoma maelekezo haya, jambo mojawapo zuri watakalogundua ni kuwa karo yetu ni ndogo. Kwanini? Hatuna michango mingi nje ya karo na karo inalipwa pole pole. Fedha nyingi iliyo nje ya karo ni ile inayohusu mahitaji yako binafsi. Mfano sare, Biblia, vyombo vya chakula, Bima, na Sayansi kwa vitendo.**

**Tunafundisha masomo ya kawaida kwa kila shule. Tunaongeza somo la Bible Knowledge na Computer. Shule yetu si ya ufundi au VETA ila kutokana na kilio cha taifa cha watoto kuhitimu bila ujuzi wowote, tuna masomo ya ujuzi mdogo mdogo kwa muda wa ziada. Utachagua mwenyewe ujuzi unaopenda. Ukishaupata ujuzi fulani, unaweza kuchagua ujuzi mwingine. Masomo ya Ujuzi ni Useremala, Saluni ya Kiume, Muziki, Kufuma, Michezo, Kushona, Fundi Bomba, Umeme, Kupamba, na Mapishi. Mkazo wetu mkubwa ni masomo ya sayansi kwa wote ingawa kwa sasa mtaala mpya unatulazimisha wanetu wachache walio na uwezo wa chini kitaaluma waache Physics na kusoma History. Tuseme, kwetu Sayansi na Hisabati "hayasomwi bali yanafanyika". Ukifika Januari 2026, utaona.**

### 1. 1 Mahali, Usafiri, na Mawasiliano

**Tuko umbali wa Kilometa 38 kutoka Manispaa ya Bukoba kwenye Halmashauri ya Bukoba. Ukitokea mjini Bukoba utapanda Hiace ziendazo uelekeo wa Izimbya, Kikomero, au Katoro. Nauli ni sh. 3,000/=. Utashuka Ibwera na kupanda pikipiki kwa sh. 1,500/= au 2,000/=. Kilometa 3 kutoka Ibwera, utajikuta umefika kilimani penye miti na upepo safi, kwenye "Bustani ya Edeni" Bukoba Hope. Utapokelewa kwa tabasamu la wanafamilia wenye upendo mwingi kwako kwa kukubali kujiunga na**

**Familia ya Washindi. Muhimu: Ukiwa na usafiri binafsi kutokea Bukoba Mjini, ukimaliza mwinuko wa Katerero, usipinde kushoto kwenda Kanazi au kulia kwenda Bujugo; nyoosha barabara ya kwenda Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Utatokea Kyema na kupinda kulia barabara kuu. Ni barabara fupi ikiwa utakuta haijafungwa kwa matengenezo.**

**Gharama za safari kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo zinalipwa na mzazi wa mwanafunzi. Hata hivyo, wakati wa kwenda na kutoka likizoni, wanetu husafiri kwa pamoja. Wanaopitia Bukoba Mjini hufikishwa kwenye magari ya kwao, na wakati wa kurudi wanetu hupokelewa TTCL Bukoba Mjini, KKKT Kagondo Rwamishenye, au Ibura. Wazazi wa mbali hawafuati na hawaleti watoto shuleni likizoni kwa kuwa tunawasindikiza na tunawapokea wenyewe. Tuko tayari kufanya mpango wa usafiri kwa mtoto tunayejulishwa kuwa atafika muda ambao magari ya abiria yameishafunga huduma hiyo mjini Bukoba, Ibura, au Kyetema.**

**Mzazi yeyote aliyeko Bukoba Mjini anayependa kutuma kitu shuleni, hufika Ujirani Mwema, Church Bookshop upande wa Karani, huacha kitu hicho hapo. Kwa hiyo mzazi anayetakakununua mahitaji ya mtoto ya darasani anaweza kununua hapo hapo dukani akaandika jina na kuwaachia.**

**2.0 MAHITAJI MUHIMU**

**2.1 Karo na Michango**

**Haijawahi kubadilika tangu mwaka 2017! Imebadilika mwaka huu 2026. Ila ili wazazi wapumue kidogo, kwa sasa tumeondoa sh. 50,000/= zilizokuwa za miundombinu. Kwa hiyo ni kama kusema karo imepanda kwa sh. 90,000/= tu. Fedha hizi za ada ziwekwe benki.**

**Jedwali Na. 1**

| KIPENGELE | MUHULA I | | MUHULA II | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Januari - Machi | Aprili - Juni | Julai - Agosti | Sept. - Novemba | Mwaka |
| Karo | 410,000/= | 295,000/= | 400,000/= | 295,000/= | |
| Jumla | 410,000/= | 295,000/= | 400,000/= | 295,000/= | 1,400,000/= |

 **Fedha zote ambazo haziko kwenye jedwali la ada utakazoweka benki ni hizi:**

| Jedwali Na. 2 | Msichana | Mvulana |
|---|---|---|
| **Sare ya shule (shati 3, tshirt 1, sweta 1,** tracksuit 1, suruali/sketi 2, | 141,000.00 | 141,000.00 |
| Kitambulisho | 5,000.00 | 5,000.00 |
| *Practicals za Sayansi | 30,000.00 | 30,000 |
| Kitabu ibada | 3,000.00 | 3,000.00 |
| Vyombo chakula | 8,000.00 | 8,000.00 |
| Alama nguo | 7,000.00 | 7,000.00 |
| *Fomu ya kujiunga (ikiwa hukufanya mtihani) | 10,000.00 | 10,000.00 |
| **JUMLA** | **204,000.00** | **204,000.00** |

***Practicals sh. 30,000/= ni kwa ajili ya kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo vingi na kufanya mitihani ya mihula kwa vitendo sawa na wafanyavyo Kidato cha Nne wanapofanya mitihani ya NECTA. Hii ni kuanzia Kidato cha I.**

Jedwali Na. 3

**Jedwali hili hela yake iletwe shuleni ikiwa huna kitu husika. Sketi/suruali ni shuleni tu.**

| | | |
|---|---|---|
| **Matokeo la 7(ikiwa huna)** | **1,000.00** | **1,000.00** |
| **Biblia RSV (Ikiwa huna. Ila lazima iwe RSV)** | **18,000.00** | **18,000.00** |
| ***Bima NHIF** | **50,400.00** | **50,400.00** |
| **Sketi/Suruali (ya ibada na matukio maalum)** | **25,000.00** | **20,000.00** |
| **JUMLA** | **94,400.00** | **89,400.00** |

***Bima ya NHIF hulipwa kila mwaka. Ni fedha za serikali. Shule haibaki na senti. Bima ni lazima kwa kila mtoto ili tuwe na uhakika wa afya ya mtoto. Bima hii imesaidia wanetu kutibiwa hadi Muhimbili !**

***Mtoto anayeanza Kidato cha I, ambaye hana vifaa vinavyotakiwa kwenye Jedwali Na. 3, ili amalize malipo yote ya mwaka, mzazi ataandaa kwa Msichana jumla sh. 1,698,400/= na Mvulana sh. 1,693,400/=. Atabaki kusubiri kujulishwa michango ya sherehe shuleni na ile ya michezo au mitihani ambayo hupangwa baadaye na shule au mamlaka nyingine.**

**Fedha zinazowekwa benki tumia Tawi lolote la CRDB, au FAHARI HUDUMA (mwenye mashine inayoandika jina la mwanafunzi). Jina la akaunti ni BUKOBA HOPE LUTHERAN SEC. A/C. Na. 0150285841800. Leta hati ya malipo "Pay-in-slip" ikiwa na jina la mwanafunzi na kidato chake vilivyoandikwa na benki kwa mashine. SHULE INA FAHARI HUDUMA. UNAWEZA KULETA FEDHA UKAWEKA BENKI HAPA SHULENI.**

**Muhimu sana**

**(i) Kuna shule nyingi zinaitwa 'Bukoba'. Hii uliyochaguliwa ni Bukoba Hope. (ii) Mtoto akiacha masomo hapa shuleni kwa sababu zake binafsi hatarudishiwa fedha ya ada kutoka shuleni isipokuwa tu kama atakuwa amelipa fedha inayozidi muhula husika (si awamu husika). Hii ni kwa kuwa awamu zilizotengwa hazimaanishi gharama za kipindi husika bali kurahisisha mzigo wa ulipaji kwa mzazi.**

**(iii) Mwanafunzi ambaye atatunziwa nafasi ni yule aliyetanguliza ada kuanzia sh. 100,000/= akatuma bank slip. Fedha hii haitarejeshwa asipojiunga na Familia yetu.**

**2.2 Mahitaji Mengine ya shule**

- **Rimu mbili za karatasi A4 zisizo na mistari. Waweza kuleta moja Januari, nyingine Julai.**
- **Matokeo yako ya Darasa la Saba: Ukiyapata shuleni yathibitishwe na Mwl. Mkuu au Kiongozi mwingine wa Elimu. Ukiyapata mtandaoni hayahitaji kuthibitishwa isipokuwa tu ikiwa hayatakuwa na jina lako.**
- **Fyekeo moja (usilete kotama).**
- **Mpini mmoja wa jembe kwa kuwa majembe tunayo.**
- **Mfagio wa nje wenye mpini (chelewa yenye mpini).**
- **Nakala ya cheti cha kuzaliwa maana kuna wanafunzi wanachanganya tarehe zao za kuzaliwa. Ikiwa huna leta cheti cha dini cha kubatizwa au cheti cha kliniki.**

**2. 3 Mahitaji Binafsi**

- ✓**Biblia ya Kiingereza iitwayo RSV ni lazima sana.**
- ✓**Fedha ya kuweka alama kwenye nguo zako ikiwa utaleta nguo zaidi ya tulizoagiza za kuvaa na kulalia. Kila nguo utaleta sh. 500/=. Nguo za kushindia weka alama mwenyewe nyumbani. Alama hii iwekwe sehemu ambayo akivaa itaonekana vizuri. Mfano eneo la mkanda mbele.**
- ✓**Kamusi kubwa ya Kiingereza tu (hasa inayoanzia bei ya sh. 25,000/= inayoitwa Students Dictionary. Ila uinunue usilete hela shuleni)**
- ✓**Mfuko wa kubebea madaftari**
- ✓**Nguo za ndani na nguo za kuvaa ili kulala.**

**Muhimu:**

**(i) Msichana lazima awe na nguo nyepesi, nyeupe au nyeusi (isiwe t-shirt), isiyo na maandishi wala picha, ya kuvaa ndani ya shati.**

BUKOBA HOPE LUTHERAN SECONDARY SCHOOL (BUHOLUSE)
ELCT - NORTH WESTERN DIOCESE
P.O. Box 1425, Bukoba, Tanzania; **Phone**: +255 754 264 200/+255 28 222 0027
**Email**: bhl.nwdelct@gmail.com **Website**: www.bukobahopelctnwd.ac.tz
**Motto:** Where Everyone is in Christ, Everyone Wins

**(ii) Mvulana ikiwa atapenda kuleta nguo ya kuvaa ndani ya shati, basi iwe nguo nyepesi nyeupe au nyeusi (isiwe t-shirt) isiyo na maandishi wala picha.**

- ✓**Kandambili (yeboyebo)**
- ✓**Taulo (Ila msichana anaruhusiwa pia kuleta kitenge kimoja au khanga moja) ✓ Sabuni za kutosha**
- ✓**Mafuta ya kujipaka**
- ✓**'Toilet paper' za kutosha (utazitunza mwenyewe)**
- ✓**Sanduku imara lenye kufuli (wengi huleta ya bati)**
- ✓**'Box file' moja kwa ajili ya kutunzia kazi zako (utalitunza wewe)**
- ✓**Mkebe wa Hesabu, rula ya inchi 12, kalamu za wino wa bluu au mweusi, na kalamu za risasi**
- ✓**Madaftari makubwa (counter book Q. 2 au zaidi) 12. Leta na madaftari mengine madogo ya kutumia unapojisomea binafsi.**
- ✓**Daftari ziitwazo 'Graph pads' 2 au zaidi (utazitunza mwenyewe kwa kazi binafsi za kitaaluma).**

**KARO NAFUU KULIKO WENGINE KWA SABABU:**

- **Matibabu kwa Huduma ya Kwanza shule inanunua dawa huchangii.**
- **Ukiugua tukakupeleka kutibiwa vituo jirani au hospitali za hapa Bukoba, shule italipa nauli yako na nauli ya mfanyakazi atakayekusindikiza. Ukilazwa, mfanyakazi au mwanafunzi atabaki kukuhudumia hadi wazazi wafike. Kawaida hatuiti mzazi kabla sisi hatujampeleka mtoto hospitalini. Hii ni kwa kuwa sisi ndiyo Familia ya mtoto akiwa shuleni.**
- **Hatuombi litokee lakini mtoto ukifiwa na mzazi, mlezi, kaka, au dada, ukiwa wa karibu tutakusindikiza. Ukiwa wa mbali, mfanyakazi atakusindikiza, shule italipa nauli yote ikiwemo hata ya kurudi kwako na matumizi ya njiani. Haya ndiyo maisha ya Kifamilia.**
- **Baba au Mama akifiwa na Mzazi wake (Babu au Bibi yako), shule itatoa rambirambi ya sh. 50,000/=**
- **Utapewa haya ikiwa ni shukrani kwa kuichagua Familia ya Washindi : ndoo, jembe, chandarua, godoro, kiti, na meza. Hauchangii fedha.**

  **Ila mtoto anayekojoa kitandani ni lazima alete godoro lake imara, Super Banco, au jingine au aina nyingine, lisilo chakavu. Godoro ni futi 2.5 kwa futi 6. Asipolileta atapewa letu kisha atanunua baadaye.**
- **Mzazi anaweza kuomba kuwa na awamu zake za kulipa ada kadri ya uwezo wake ilimradi amalize ada yote tarehe 15/11/2026. Hata hivyo, mzazi hawezi kukaa kimya bila kulipa ada akisubiri mwishoni maana lazima tuishi kwa ada hiyo. Mzazi anayeomba awamu zake aandike barua ya kuomba ikionesha awamu zake na aje nayo siku akimleta mtoto. Njia hii inawalenga hasa wazazi wenye shida kubwa mno ya kipato.**


## 2.4 Sare ya Shule (haipatikani shuleni)

| | |
|---|---|
| **MSICHANA MVULANA** | |
| **Soksi nyeupe zisizo na matundu jozi 3 vilivyofunikwa vyenye visigino Viatu vyeusi visiwe simple au bajaji visigino vifupi (sentimeta** | **Soksi nyeupe zisizo na matundu jozi 3 Viatu vyeusi vilivyofunikwa vyenye vifupi (sentimeta 2) – 2) – si mchongoko.** |
| **Sketi 1 dark blue – solo ambayo ukikaa Suruali moja (1) dark blue isiyobana na isifunue magoti. Njoo umeivaa siku ya isiyoacha kiuno wazi ukiinama. Shona na njoo kuripoti. umeivaa siku ya kuripoti.** | |
| **T-Shirt 2: nunua rangi ya njano zisizo na T-Shirt 2: nunua rangi ya kijani zisizo na maandishi yoyote wala kola. (Vaa moja maandishi yoyote wala kola. (Vaa moja wakati wakati wa kuripoti shuleni). wa kuripoti shuleni). Kijani yenye giza/weusi hapana** | |
| **Bukta nyekundu kwa ajili ya michezo (isiyombana sana)** | **Bukta ya bluu kwa ajili ya michezo.** |
| | |

| **MSICHANA** | **MVULANA** |
|---|---|
| ~~**Raba kwa ajili ya michezo.**~~ | ~~**Raba kwa ajili ya michezo.**~~ |
| ~~**Jozi moja ya viatu rahisi 'Simple open shoes'**~~ | ~~**Jozi moja ya 'Simple open shoes'**~~ |

✓ **Viatu vinavyokubalika kwa Kaka na Dada na Biblia ya RSV ni hivi kwenye picha:**





**2. 5 Malazi ○ Mto 1, foronya 2 (moja bluu bahari na nyingine pinki), blanketi 1, na mashuka 2 (moja pinki na jingine bluu bahari). Muhimu: Shuka liwe refu kiasi cha kukunjiwa chini ya godoro kichwani na miguuni. Huu ni urefu usiyo chini ya mita 2 na robo. Shuka dogo sana linasababisha ngozi ya mtoto kugusa godoro. Kiafya si sahihi.**

***Mahitaji ya mavazi na malazi tumeweka idadi ila mtoto unaweza kuleta au kulipia idadi zaidi ya tuliyotaja kadri ya uchumi wa familia.**

**2.6 Vifaa Utakavyoazima Shuleni**

**Kila kifaa utakachoazima au kukabidhiwa shuleni itakubidi ukitunze vizuri. Kikiharibika au ukikipoteza utalazimika kukilipia. Kwa kawaida ukiharibu au kupoteza kitu kimoja, utalipa viwili isipokuwa kitabu utalipia tu idadi uliyoharibu au kupoteza.**

***** Maelekezo haya yenye sahihi ya Mkuu wa Shule ni kwa ajili tu ya wanafunzi ambao tayari wamechaguliwa na kuandikwa kwenye orodha ya waliofaulu shuleni.**

**Tunakutakia maandalizi mema na safari njema. Karibu sana kwenu tujenge Familia moja ya Washindi. Tunakusubiri kwa shauku kwa sababu tunakupenda (We love you).**

**Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi**
**MKUU WA SHULE 0754 264 200 / 0759742310 / 0756840347**

## SHERIA ZA SHULE

### 1. NIDHAMU, MAADILI, NA IBADA

**Hongera kwa kuchagua Bukoba Hope Lutheran 'kijito cha malezi'. Kwetu ukweli, kuabudu, uaminifu, upendo, amani, uwajibikaji, na ufanisi ni tunu mama. Kwa hiyo, pamoja na kwamba umetumiwa sheria za shule, ni muhimu kuzingatia tunu hizi moyoni mwako na kuzifuata bila shuruti maana ndizo msingi wa sheria ulizopewa. Unapaswa kuhudhuria sala na ibada bila kulazimishwa. Familia ya Bukoba Hope inatambua kuwa 'maisha ni ibada'.**

### 2. USAFI

**Unatakiwa kuwa nadhifu wakati wote. Nguo za heshima, usafi wa mwili na roho, na kutunza mazingira. Tunatamani ukirudi nyumbani familia yako na jamii wakuone mwema kitabia na kitaaluma.**

### 3. TAALUMA NA LUGHA RASMI

**Umeamua kujiunga na Bukoba Hope kwa lengo kuu moja, yaani kujifunza. Sharti ufanye jitihada katika taaluma, uhudhurie vipindi, uwahi darasani, uwe makini mwalimu anapofundisha, uulize maswali usipoelewa, usitoroke, ufanye mazoezi na majaribio yote unayopewa. Huruhusiwi kupiga kelele au kuwasumbua wenzio darasani. Alama za ushindi kwa kila somo ni 55%. Ukipata alama za chini itakubidi ama urudie mtihani, urudie darasa, au uhamie shule nyingine. Hata hivyo, hatutegemei ushindwe mitihani kwa kuwa tunawekeza sana katika kuwasaidia wanetu wenye kukwama kitaaluma ilimradi isiwe kwa uzembe wako.**

**Unapaswa kutumia lugha ya Kiingereza wakati wote ukiwa hapa shuleni kwa sababu tunakuandaa uwe msomi wa Kimataifa. Licha ya kuwa lugha rasmi ya mawasiliano, Kiingereza ni lugha inayotumika kufundishia masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili na Maadili. Usipoongea Kiingereza kwa hiari, tutakulazimisha. Ikiwa umesoma shule zinazotumia Kiswahili kufundishia, baada ya miezi 6 utakuwa unaongea Kiingereza kama uliyesoma 'English Medium'!**

### 4. MKATE WA KILA SIKU

**Kabla hujaanza safari kuja shuleni, tafuta Biblia ya Kiingereza, kaa na familia yako, chagua mstari mmoja mfupi, uandike ulivyo kwa Kiingereza. Anza kuukariri ili liwe Neno la Mungu la msingi katika maisha yako. Hivyo chagua mstari unaozungumza nawe na kukuelekeza vema. Kila nusu muhula tunakuwa na mstari wa Biblia wa kuiongoza familia yetu. Basi, mkate wetu wa kila siku ni Neno la Mungu.**

### 5. UVAAJI NA VIPODOZI SHULENI

**i) Wakati wa masomo au unaporuhusiwa kutoka nje ya shule unapaswa kuvaa sare ya shule.**
**ii) Baada ya masomo unapaswa kuvaa sare ya shughuli za nje ya darasa au sare ya michezo wakati wa michezo. Hakuna nguo nyingine ya nyumbani inavaliwa shuleni labda kwa kibali maalum sana.**
**iii) Wakati wa mahafali utapaswa kuvaa sare maalum ya shule.**
**iv) Huruhusiwi kutumia vipodozi na marashi ukiwa shuleni isipokuwa kwa hitaji maalum.**

**6. KUTEMBELEWA NA WAGENI SHULENI**

**Utaruhusiwa kutembelewa na wazazi/walezi au jamaa walioorodheshwa kwenye fomu iliyoambatishwa hapa kwa tarehe itakayotangazwa. Utaruhusiwa kuongea na wageni wako kwenye sehemu iliyoandaliwa kwa mapokezi tu. Wageni wako wavae kiheshima wanapokuja shuleni. Siku ya kukutembelea, wataleta vitu kadri shule itavyoelekeza. Nitaje vya msingi visivyoruhusiwa ni kama wali, pilau, ndizi, na pombe. Hata hivyo, siku hiyo wakileta zawadi yako, wanatakiwa kutenga pia zawadi kwa ajili ya familia nzima, kwa maana si watoto wote hutembelewa. Ndiyo maana ya Maisha yetu ya kifamilia.**

**7. KWENDA NJE YA SHULE**

**Ukiwa na shida ya kukulazimisha kwenda nje ya shule sharti uombe ruhusa na kupewa kibali maalum. Ni kosa kwenda nje ya shule bila ruhusa na karatasi ya kibali.**

**8. MISEMO AU KAULI ZA MALEZI SHULENI**

- **Tunasema tumia hekima au busara katika maamuzi nyeti hata kama kuna sheria au hakuna sheria.**
  **Ma Badi: Ufupi wa jina la mwanamke mmoja Marehemu Baldiana Ngeiyamu aliyewalea wanae akiwambia kuwa kuna mambo mawili ya lazima katika maisha lakini hayafundishwi shuleni, ni haya kwa Kiingereza: Common sense na Sense of responsibility (Kiswahili tuseme ni Akili ya kuzaliwa na Moyo wa kujituma). Ukiambiwa tu Ma Badi utaelewa haraka kilichokushinda kati ya hayo mawili.**
- **SHULE POLE POLE – Maana yake ukiwa mgeni, kwanza tulia ili ujifunze tunavyoishi.**
- **SISI NI FAMILIA YA WASHINDI ukilenga ushindi wa tabia na kitaaluma.**
- **SI MZITO, NI MDOGO WANGU**
- **ALONE YOU GO FAST, TOGETHER YOU GO FAR**
- **Neno la Mungu kwenye mazingira yetu: Mf: FOR GOD'S TEMPLE IS HOLY, AND THAT TEMPLE YOU ARE. Lengo ni kumtaka kila mwanafamilia kulinda mwili wake usichafuke kiroho. Misemo hii ni muhimu sana kuliko sheria katika kujenga familia yetu.**

**9. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFANYA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE**

**(i) Kukiuka sheria za shule.**
**(ii) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya wenzake.**
**(iii) Kuwagomea viongozi.**
**(iv) Kuwatukana au kuwapiga wenzako na watu wengine.**
**(v) Ulevi, uvutaji wa sigara, bangi au utumiaji wa madawa ya kulevya (vi) Uasherati**
**(vii)Wizi**
**(viii) Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule.**
**(ix) Utoro wa aina yoyote kama vile kutokuwemo darasani unapotakiwa kuwa darasani, kutoka nje ya shule bila kibali, na kwenda sehemu tofauti na uliyoruhusiwa kwenda.**
**(x) Kuwa na simu, redio au kamera shuleni. Mawasiliano yote yatapitia kwa Mkuu wa Shule au atakayepewa jukumu hilo na Mkuu wa Shule.**
**(xi) Udanganyifu kwenye mitihani na majaribio. Adhabu yake ya haraka ni kurudishwa nyumbani kwanza kwa siku zisizopungua 21. Bukoba Hope hatutazamii mitihani ya ndani au ya nje.**
**(xii) Kushindwa kutumia hekima na busara katika maamuzi nyeti.**

**Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi**
**MKUU WA SHULE 0754 264 200 / 0759742310/ 0757040188/ 0768530225**

**BUKOBA HOPE LUTHERAN SECONDARY SCHOOL (BUHOLUSE)**
ELCT - NORTH WESTERN DIOCESE
P.O. Box 1425, Bukoba, Tanzania; **Phone**: +255 754 264 200/+255 28 222 0027
**Email**: bhl.nwdelct@gmail.com **Website**: www.bukobahopelctnwd.ac.tz
**Motto:** Where Everyone is in Christ, Everyone Wins

**TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI**

**1. HISTORIA YA MWANAFUNZI**
**Jina la mwanafunzi ……………………………….........................................................................**
**Tarehe ya kuzaliwa ……………………………….....................................................................**
**Kijiji/Mtaa……………………........................Wilaya…………........…………......Mkoa …..............….**
**Shule aliyohitimu darasa la VII ………………....……..................... Wilaya……...…..................**
**Mkoa…....……..............................**
**Mwaka wa kuhitimu Elimu ya msingi ................................. Daraja lako la ushindi darasa la saba: ..........................................................**

**Sekondari ya serikali uliyopangiwa ............................................ Wilaya ................................…. Mkoa ...............................................**

**Dini yako: Mwislamu/Mkristo (kata mojawapo)**
**Madhehebu: Kilutheri/Roman/Anglican/Moravian/Shiha/ au ………………………………….........**

**2.0 FAMILIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)**
**2.1. Mzazi /Mlezi**
**Jina la Baba/Mlezi ……………….......................................….......................... Simu: ........................**
**Jina la Mama/Mlezi ………………………………………... Simu…..................…………………...**
**Kazi ya Baba/Mlezi....................................................................Kazi ya Mama/Mlezi…………… Anwani ya Posta: ……..............…………………………………......................................................**
**Dini au Madhehebu ya wazazi: Baba ………………………….............. Mama: ......................... Kabila la Baba (linahitajika katika kitabu cha usajili wa wanafunzi): ..........................................**

**2.2 Ndugu au marafiki wa familia**
**Tafadhali jaza majina ya ndugu/marafiki wa familia wasiozidi 4 wanaoruhusiwa kumtembelea au kushirikishwa raha, shida au hitaji la mtoto akiwa shuleni. Mzazi ukiwa mbali ila una jamaa wa karibu na shule ni vyema kumuandika huyo. Hapa usiandike jina la baba au mama au mlezi maana hao tayari wameandikwa juu.**

| JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**3. TAARIFA YA PEKEE YA MZAZI NA AHADI**

**Je, mzazi, mwanetu ana tabia mbaya yoyote unayopenda tumsaidie? Kama anayo eleza na ikibidi ushauri asaidiweje. ……………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………**

**4. KUKUBALI MAELEKEZO NA KUJIUNGA NA SHULE**
**(Ijazwe na mwanafunzi na mzazi baada ya kusoma na kuelewa vema maagizo ya kujiunga)**
**Baada ya kusoma na kuelewa maagizo ya kujiunga na BUKOBA HOPE LUTHERAN**

**Mimi …………………...............................................................................................................**
**ninaahidi kuwa nitafuata sheria za shule na maagizo mengine yatakayotolewa na uongozi wa shule.**

**………………………...............** ………………….
**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

**Baada ya kusoma na kuelewa maagizo ya mwanangu kujiunga na Bukoba Hope Lutheran, ninamruhusu kujiunga na shule hii. Ninaahidi kumtimizia mwanangu mahitaji ya shule ili ajiunge na kuendelea na masomo shuleni hapa Bukoba Hope Lutheran.**

**………………………………** **……………………….**
**Jina la Mzazi/Mlezi** **Saini ya Mzazi/Mlezi**
**Tarehe…………….**

*************************************************************************************************************
*************************************************************************************************************
**********

## 5. AFYA YA MWANAFUNZI

**Mimi Dr/Tabibu ………………………………………………………………………..**
**wa Hospitali ya au Kituo cha Afya cha …………………………………………**
**nimempima afya (Jina la mwanafunzi) …………………………………………**
**na nimebaini ana/hana ugonjwa (taja ugonjwa kama anao) ………………**
**…………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………...Ushauri wa Daktari/Tabibu: …….**
**…………………………………………………………………………………………**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………….
**SAHIHI YA DAKTARI/TABIBU**
**NA MHURI**

***Ikiwa mtoto amekwishapimwa afya kwa kutumia fomu ya shule nyingine, asipimwe tena ila badala yake alete fomu ya shule nyingine yenye taarifa ya afya yake.**

**Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi**
**MKUU WA SHULE 0754 264 200**